# HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 39 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Julai 2026

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA


# CHONGOLO: SOGEZENI MBOLEA KWA WAKULIMA



Waziri wa Kilimo, Mhe. Daniel Chongolo (Mb), akizungumza na wananchi wa Mang'ola, katika Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, wakati wa ziara yake ya kikazi na ukaguzi wa miradi ya maendeleo mkoani Arusha.


NDANI>>

ELIMISHENI WAKULIMA MATUMIZI SAHIHI YA MBOLEA, HIMIZENI MBOLEA HAI 3





USHIRIKIANO WA TFRA NA NAESA KUONGEZA TIJA NA UZALISHAJI WA MAZAO YA KILIMO NCHINI 5

# CHONGOLO: SOGEZENI MBOLEA KWA WAKULIMA

Waziri wa Kilimo, Mhe. Daniel Chongolo (Mb) meiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima kwa wakati, ikiwemo wakulima wa Kijiji cha Mang'ola, Wilaya ya Karatu mkoani Arusha.

Waziri Chongolo alitoa agizo hilo tarehe 22 Julai, 2026 wakati wa ziara yake ya kikazi iliyolenga kukagua miradi ya maendeleo na kusikiliza changamoto zinazowakabili wananchi, hususan wakulima mkoani humo.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, alisema wakulima wataendelea kupatiwa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mbolea kupitia Kampeni ya Mali Shambani, inayoratibiwa na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Mamlaka kuanza mwezi Agosti 2026.

Alisema matumizi sahihi ya mbolea hayapaswi kuangaliwa kwa msingi wa kununua mbolea kwa jina pekee, bali mkulima anapaswa kupewa elimu ya kuchagua na kutumia mbolea kulingana na mahitaji ya virutubisho vya udongo, afya ya udongo na aina ya mbegu.

"Matumizi mbadala si kununua mbolea kwa jina, badala yake ni kuwa na elimu sahihi ya matumizi ya mbolea kwa kuendana na virutubisho, afya ya udongo na mbegu bora," alisema Laurent.



Waziri wa Kilimo, Mhe. Daniel Chongolo (Mb), akizungumza na wananchi wa Mang'ola, katika Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, wakati wa ziara yake ya kikazi na ukaguzi wa miradi ya maendeleo mkoani Arusha.

Kuhusu biashara holela ya mbolea, Bw. Laurent alisema TFRA haitamruhusu mfanyabiashara kuuza mbolea kinyume na masharti ya leseni yake, akisisitiza kuwa miongoni mwa hatua za kinidhamu kwa watakaokiuka masharti ni kufutiwa leseni.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mbolea Tanzania (TFC), Bw. Samwel Mshote, alisema tani 2,000 za mbolea aina ya DAP zitapelekwa Mang'ola ndani ya wiki mbili ili kukidhi mahitaji ya wakulima.

Alisema pia taratibu zinaendelea kuhakikisha wakala wa mbolea Mang'ola anapatikana, hatua itakayowawezesha wakulima kupata mbolea kwa urahisi sambamba na elimu kuhusu matumizi yake sahihi.

Serikali pia imeendelea kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbolea kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa, kwa lengo la kuhakikisha wakulima wanapata mbolea kwa bei himilivu na kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao.

# Elimisheni wakulima matumizi sahihi ya mbolea, himizeni mbolea hai

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Peter L. M. Msoffe, ameielekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kuendelea na utoaji wa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya mbolea na kuhamasisha matumizi ya mbolea hai ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao, kuboresha afya ya udongo na kuendeleza kilimo endelevu nchini.

Prof. Msoffe alitoa maelekezo hayo leo tarehe 3 Julai, 2026 alipotembelea banda la TFRA katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yanayoendelea katika Viwanja vya Julius Nyerere.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Peter L.M. Msoffe akizungumza katika banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) alipotembea banda hilo katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere.

Akiwa bandani hapo, alielezwa kuhusu huduma zinazotolewa na TFRA, zikiwemo utoaji wa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mbolea, utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku ya Mbolea, hamasa ya kupima afya ya udongo, uhamasishaji wa matumizi ya mbolea hai na utoaji wa taarifa kuhusu fursa za uwekezaji katika tasnia ya mbolea.




Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo wa Wizara ya Kilimo, Prof. Peter. L. M. Msoffe akipewa maelezo na Meneja wa TFRA Nyanda za Juu Kusini, Joshua Ng'odya alipotembelea banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) katika maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Sabasaba), yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere.

Prof. Msoffe alipongeza TFRA kwa juhudi zake za kusimamia tasnia hiyo na kuendelea kuwahudumia wakulima pamoja na wadau wengine wa kilimo kwa kutoa huduma zinazochangia kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuendelea kuhamasisha matumizi ya mbolea hai zinazotokana na malighafi za asili, ikiwemo mkojo wa sungura na vyanzo vingine vya kikaboni, akieleza kuwa matumizi yake yanasaidia kuboresha rutuba ya udongo, kuongeza uzalishaji wa mazao na kuchangia uhifadhi wa mazingira kupitia kilimo endelevu.

Kwa upande wake, TFRA inaendelea kutumia Maonesho ya Sabasaba kama jukwaa muhimu la kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu tasnia ya mbolea ikiwa ni pamoja na fursa za uwekezaji na biashara ya mbolea.

# Elimisheni wakulima matumizi sahihi ya mbolea, himizeni mbolea hai



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Prof. Peter L. M. Msoffe akisaini kitabu cha wageni alipotembea banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) katika maonesho ya katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere.

# Ushirikiano wa TFRA na NAESA kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini

Ushirikiano baina ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) na Wakala wa Taifa wa Huduma za Ugani Kilimo (NAESA) unatarajiwa kuimarisha huduma za ugani, kuongeza matumizi sahihi ya mbolea na hatimaye kuinua tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo nchini.

Hayo yalibainishwa wakati wa kikao cha pamoja baina ya Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, na Kaimu Mtendaji Mkuu wa NAESA, Dkt. Wilhelm Leonard Mafuru, kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi za NAESA, NANENANE-Nzuguni, jijini Dodoma.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Joel Laurent, alisema taasisi hizo zina majukumu yanayokamilishana katika kuendeleza sekta ya kilimo na kwamba ushirikiano huo utaimarisha utoaji wa huduma kwa wakulima nchini.

Laurent alisema ushirikiano huo utajumuisha utoaji wa mafunzo kwa maafisa ugani, uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea, uanzishwaji wa mashamba darasa na utoaji wa elimu kuhusu afya ya udongo ili kuongeza tija ya uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza kipato cha wakulima.

Kwa upande wake, Kaimu Mtendaji Mkuu wa NAESA, Dkt. Wilhelm Leonard Mafuru, amesema ushirikiano huo utafungua ukurasa mpya wa kuimarisha utendaji wa taasisi hizo kwa lengo la kumfikia mkulima moja kwa moja kupitia huduma bora za ugani.

Dkt. Mafuru amesema matumizi ya mifumo ya pamoja yatawawezesha maafisa ugani kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kuongeza ushirikiano katika utoaji wa elimu, maarifa na ubunifu utakaochangia kuongeza tija katika sekta kilimo Viongozi hao walisisitiza kuwa ushirikiano kati ya TFRA na NAESA utakuwa nguzo muhimu ya kuhakikisha wakulima wanapata huduma bora za ugani, mbolea zenye ubora unaotakiwa pamoja na elimu ya matumizi sahihi ya mbolea, hatua itakayochangia maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo nchini.




Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent (wa tatu kulia), na Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Taifa wa Huduma za Ugani Kilimo (NAESA), Dkt. Wilhelm Leonard Mafuru (wa nne kushoto), wakiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TFRA na NAESA baada ya kikao cha kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi hizo, kilichofanyika katika Ofisi za NAESA, Nzuguni, jijini Dodoma tarehe 27 Julai, 2026.

# USHIRIKIANO WA WADAU WATAJWA KUONGEZA TIJA YA UZALISHAJI MAZAO YA KILIMO



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, akipewa maelezo katika banda la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) alipotembelea banda hilo katıka Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.

Imeelezwa kuwa, zao la ufuta ni miongoni mwa mazao yanayohitaji matumizi makubwa na sahihi ya mbolea ili kuongeza tija ya uzalishaji na kuboresha ubora wa mavuno.

Mtaalamu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ametoa maelezo hayo mbele ya Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, alipotembelea banda hilo katıka Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.

Alibainisha kuwa, wakulima wengi wa kusini mwa Tanzania hufanya kilimo cha kuhamahama kutafuta maeneo yenye rutuba badala ya kutumia mbolea kutokana na mazoea ambapo wakitumia mbolea kwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu wataongeza uzalishaji wa zao hilo pamoja na kuongeza thamani yake bila kuadhiri eneo la makuzi ya watoto kutokanako na kuhamahama.

Akizungumza baada ya kutembelea mabanda ya taasisi mbalimbali yaliyoshiriki maonesho hayo, Mkurugenzi Mtendaji, Laurent, alisema ushirikiano miongoni mwa taasisi za utafiti, sekta binafsi na wadau wa kilimo ni msingi muhimu katika kuimarisha matumizi sahihi ya mbolea, kuongeza uwekezaji na kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

Laurent alisema TFRA itaendelea kushirikiana na TARI katika kuhamasisha matumizi sahihi ya mbolea ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao ya kimkakati, ikiwemo ufuta.

Katika banda la Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), Meneja wa Mradi wa taasisi hiyo, Peter Mwangalo, alimueleza Laurent kuhusu juhudi zinazofanywa katika kuhamasisha kilimo endelevu na matumizi ya mbolea za asili.

Akiwa ndani ya banda la TPHPA, Laurent alielezwa Laurent tofauti kati ya mbolea za maji na viuatilifu kuwa, mbolea hutoa virutubisho vinavyohitajika kwa ukuaji wa mimea, wakati viuatilifu ni sumu iliyoandaliwa maalum kwa ajili ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao.

Pamoja na mabanda hayo, Laurent alitembelea banda la Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC),Tume ya Maendeleo ya Ushirika ikiwa ni sehemu ya juhudi za TFRA za kuimarisha ushirikiano na wadau wa tasnia.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) , Joel Laurent, ( Katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Mamlaka hiyo alipotembelea banda la Mamlaka katika maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba) yaliyofanyika Jijini Dar es salaam.

# Mkurugenzi Mkuu COPRA apongeza ushirikiano baina ya Taasisi za Wizara ya Kilimo




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Irene Mlola, akipewa maelezo na Meneja wa TFRA Nyanda za Juu kusini Joshua Ng'odya namna mbolea za maji zinavyopaswa kutumia na jinsi TFRA inavyozisajili alipotembelea banda la TFRA katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Sabasaba), yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere Jijini Dar es salaam.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao mchanganyiko (COPRA), Irene Mlola, alipongeza ushirikiano baina ya COPRA na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) unaopelekea kuboresha utoaji wa huduma kwa wakulima na wadau wengine wa sekta ya kilimo.

Alieleza kuwa ushirikiano kwa karibu baina ya taasisi hizo unawawezesha kutekeleza kwa ufanisi zaidi majukumu yao ya kuwahudumia wakulima na kuchochea maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

Mlola alitoa kauli hiyo alipotembelea banda la TFRA katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere jijini Dar es salaam.

Aidha, Mlola alipongeza TFRA Kwa kazi kubwa inayofanya katika kusimamia tasnia ya mbolea na kuhakikisha wakulima pamoja na wadau wa sekta hiyo wanapata huduma stahiki.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Irene Mlola, akipewa maelezo na Meneja Uhusiano, Mawasiliano na Elimu wa TFRA, Matilda Kasanga kuhusu huduma zitolewazo na Mamlaka alipotembelea banda la Mamlaka katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Sabasaba), yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere Jijini Dar es salaam.

# KAMISHNA WA MAGEREZA KAVIRONDO AIPONGEZA TFRA KWA ELIMU YA MBOLEA WANAYOITOA



Kamishna wa Magereza, C.P.A. J. Kavirondo, akizungumza katika banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) alipotembelea banda hilo katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Sabasaba) katika Viwanja vya Julius Nyerere Jijini Dar es salaam.

Kamishna wa Magereza, C.P.A. J. Kavirondo, ametoa pongezi kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa kuendelea kutoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mbolea na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mbolea za Ruzuku kwa wakulima nchini.

Akizungumza alipotembelea banda la Mamlaka katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba 2026), Kamishna Kavirondo alisema ushirikiano uliopo kati ya Jeshi la Magereza na TFRA umechangia kuimarisha shughuli za kilimo zinazofanywa na jeshi hilo kwa kuhakikisha upatikanaji wa mbolea bora na matumizi yake sahihi.

Aidha, aliiomba TFRA kuendelea kuimarisha ushirikiano huo ili kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao, kuwajengea uwezo wafungwa kupitia kilimo na kuchangia katika kuimarisha usalama wa chakula nchini.

Kwa upande wake, Meneja wa TFRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Joshua Ng'ondya, alimueleza Kamishna Kavirondo kuwa, TFRA inaendelea kusimamia ubora na upatikanaji wa mbolea nchini sambamba na kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea kwa wakulima na wadau wengine ili waweze kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao ya kilimo.



Kamishna wa Magereza, C.P.A. J. Kavirondo, akisaini kitabu cha wageni katika banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) alipotembelea banda hilo katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Sabasaba) katika Viwanja vya Julius Nyerere Jijini Dar es salaam.

# TOAM Yaipongeza TFRA kwa Kuendeleza Elimu ya Matumizi ya Mbolea Hai



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi inayosimamia na kuratibu maendeleo ya kilimo hai Tanzania (TOAM), Bakari Mongo, akizungumza katika banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), alipotembea katika banda hilo katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Sabasaba) yaliyifanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere Jijini Dar es salaam.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi inayosimamia na kuratibu maendeleo ya kilimo hai Tanzania (TOAM), Bakari Mongo, ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa kuendelea kuhamasisha matumizi ya mbolea hai kwa wakulima na wadau nchini.

Ametoa pongezi hizo alipotembelea banda la Mamlaka katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), ambapo alipata maelezo kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Mamlaka pamoja na juhudi zake za kuhamasisha matumizi sahihi ya mbolea, ikiwemo mbolea hai.

Mongo alisema kuwa jitihada za Mamlaka katika kutoa elimu kuhusu matumizi ya mbolea hai ni muhimu katika kukuza kilimo endelevu, kulinda afya ya udongo na kuongeza uelewa wa wakulima na wadau kuhusu matumizi sahihi ya mbolea.

Kwa upande wake, Meneja wa TFRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Joshua Ng'ondya, alisema kuwa utoaji wa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mbolea ni miongoni mwa majukumu ya msingi ya Mamlaka, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha matumizi ya mbolea hai.

Wadau wa tasnia ya mbolea ikiwa ni wakulima, wafanyabiashara na viongozi mbalimbali waliendelea kutembelea banda la TFRA na kupata elimu kuhusu huduma zinazotolewa na Mamlaka, pamoja na fursa mbalimbali za uwekezaji zinazopatikana kwenye mnyororo mzima wa tasnia ya mbolea nchini.




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi inayosimamia na kuratibu maendeleo ya kilimo hai Tanzania (TOAM), Bakari Mongo, akipatiwa maelezo na Meneja wa TFRA Nyanda za Juu Kusini, Joshua Ng'odya alipotembelea katika banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Sabasaba) yaliyifanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere Jijini Dar es salaam.

# TFRA KUIMARISHA USHIRIKIANO NA VYAMA VYA USHIRIKA

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imeendelea kuimarisha ushirikiano na vyama vya ushirika pamoja na wafanyabiashara wa mbolea nchini ili kuhakikisha wakulima wanapata mbolea bora, kwa wakati na kwa bei himilivu.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Jeremiah Mugeta, alipotembelea banda la TFRA katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.



Mkurugenzi wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Jeremiah Mugeta, akipokea zawadi kutoka kwa Afisa Uhusiano wa TFRA alipotembelea banda la Mamlaka hiyo katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, Mugeta alipata maelezo kuhusu huduma zinazotolewa na TFRA, fursa za uwekezaji katika tasnia ya mbolea pamoja na namna Mamlaka inavyoshirikiana na vyama vya ushirika katika kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima kwa urahisi na kwa wakati.

Mugeta alisema vyama vya ushirika vina mchango mkubwa katika usambazaji wa pembejeo za kilimo, hivyo vina nafasi muhimu ya kuwa kiungo kati ya wakulima na wasambazaji wa mbolea nchini.

Alisema ushirikiano huo ni muhimu katika kuhakikisha wakulima wanapata mbolea yenye ubora unaotakiwa na inayokidhi mahitaji yao ya uzalishaji, jambo litakalosaidia kuongeza tija na kuimarisha sekta ya kilimo.

Aidha, alielezwa kuwa Serikali imejumuisha aina mbalimbali za mbolea katika Mfumo wa Ruzuku ya Mbolea, hatua inayolenga kuongeza upatikanaji wa mbolea kwa wakulima kwa bei nafuu na hivyo kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija katika kilimo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Umoja wa Wafanyabiashara wa Pembejeo Mkoa wa Njombe (UWAPENJO), Zakayo Mepuyinywe, alisema wafanyabiashara wa pembejeo mkoani humo wamejipanga kuhakikisha mbolea za aina mbalimbali zinapatikana kwa wakati ili kukidhi mahitaji ya wakulima katika msimu wa kilimo.



Mkurugenzi wa Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Jeremiah Mugeta, akipewa maelezo na Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Joshua Ng'odya, alipotembelea banda la TFRA katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yaliyofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

Mepuyinywe alipongeza ushirikiano uliopo kati ya TFRA na wafanyabiashara wa mbolea, akisema umekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha upatikanaji wa mbolea bora nchini na kuongeza imani ya wakulima katika mfumo rasmi wa usambazaji wa pembejeo.

Alisema ushirikiano kati ya TFRA, vyama vya ushirika na wafanyabiashara wa pembejeo ni muhimu katika kuhakikisha huduma za pembejeo zinawafikia wakulima kwa ufanisi, hasa katika maeneo yenye mahitaji makubwa ya mbolea.

# WAWEKEZAJI KUTOKA CHINA WAVUTIWA NA FURSA ZA UWEKEZAJI KATIKA TASNIA YA MBOLEA



Meneja wa TFRA Nyanda za Juu Kusini, Joshua Ng'odya akitoa maelezo kwa mtembeleaji wa maonesho kutoka China, Bon Chen kwenye banda la Mamlaka katika Maonesho ya 50 ya biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Sabasaba) yaliyiofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere Dar es salaam.

Wawekezaji kutoka nchini China wameonesha nia ya kuwekeza katika tasnia ya mbolea nchini kwa kuanzisha kiwanda cha kuchanganya mbolea (Blending Facility).

Akizungumza baada ya kupokea elimu kutoka wataalam wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), mmoja wa wawekezaji hao, Bon Chen, alisema amevutiwa na fursa zilizopo nchini pamoja na maelezo waliyopatiwa kuhusu taratibu za usajili wa wawekezaji na mbolea, hatua ambayo imewapa hamasa ya kundelea na mchakato wa uwekezaji.

Alisema wataendelea kushirikiana na Mamlaka kwa kufanya mawasiliano ya karibu ili kukamilisha taratibu zote zinazohitajika kwa ajili ya kuanzisha kiwanda hicho, hatua itakayochangia kuongeza upatikanaji wa mbolea nchini.

Kwa upande wake, Meneja wa Mamlaka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Joshua Ng'ondya, alisema Mamlaka inaendelea kutangaza fursa za uwekezaji zinazopatikana kwenye tasnia ya mbolea nchini pamoja na kusimamia taratibu za usajili wa wawekezaji na mbolea ili kuhakikisha uwekezaji unafanyika kwa kuzingatia sheria na viwango vinavyotakiwa.

Aliongeza kuwa, TFRA itaendelea kuwahudumia wawekezaji kwa kuwapatia taarifa na mwongozo unaohitajika ili kuvutia uwekezaji zaidi katika tasnia ya mbolea na kuchangia mandeleo ya sekta ya kilimo.



Mtembeaji kutoka China, Bon Chen akizungumza na wataalam ndani ya banda la Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), alipotembelea banda hilo katika Maonesho ya 50 ya biashara ya Kimataifa ya Dar es salaam (Sabasaba) yaliyiofanyika katika Viwanja vya Julius Nyerere Dar es salaam.

# WAKAGUZI WA MBOLEA WAASWA KUSIMAMIA UBORA KWA UADILIFU

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, amewataka wakaguzi wa mbolea nchini kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, weledi na uadilifu wa hali ya juu ili kuhakikisha mbolea zinazowafikia wakulima zinakidhi viwango vya ubora vinavyotakiwa.

Laurent alitoa wito huo wakati akifungua mafunzo ya wakaguzi wa mbolea yaliyofanyika kwa siku mbili, tarehe 6 na 7 Julai 2026 katika Hoteli ya Edema, jijini Dodoma yakilenga kuimarisha uwezo wa wakaguzi katika usimamizi na utekelezaji wa shughuli za ukaguzi wa mbolea nchini.



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya ukaguzi wa mbolea wakifuatilia mafunzo hayo yaliyofanyika katika Hoteli ya Edema jijini Dodoma.

Alisema wakaguzi wa mbolea wana nafasi muhimu katika kulinda maslahi ya wakulima kwa kuhakikisha mbolea zinazozalishwa, kuingizwa na kusambazwa nchini zinazingatia viwango vya ubora vilivyowekwa.

Aidha, aliwapongeza washiriki kwa kuteuliwa kushiriki matunzo hayo, akieleza kuwa uteuzi wao unaonesha imani kubwa waliyopewa na viongozi wao katika kusimamia kwa ufanisi tasnia ya mbolea nchini.

“Tekelezeni majukumu yenu kwa kuzingatia sheria, haki na maadili ya utumishi wa umma. Ufanisi wenu katika ukaguzi wa mbolea utachangia kuongeza tija katika sekta ya kilimo na kufikiwa kwa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050,” amesema Laurent.

Akiwasilisha mada kuhusu Sheria ya Mbolea, Afisa Sheria wa TFRA, Kassim Adam, aliwaeleza washiriki wa mafunzo kuwa Sheria ya Mbolea inaipa Mamlaka jukumu la kukagua maduka na maghala ya mbolea.

Alisisitiza kuwa ukaguzi huo unapaswa kufanyika kwa kuzingatia matakwa ya sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia tasnia ya mbolea.

Washiriki wa mafunzo haya ni wakaguzi wa mbolea haya ni wakaguzi wa mbolea kutoka mikoa 13 nchini ikiwa ni Mkoa wa Mara, Njombe, Geita, Morogoro, Mbeya, Iringa, Manyara, Kigoma, Tanga, Dodoma, Pwani, Kilimanjaro na Tabora.







Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya ukaguzi wa mbolea wakipokea vyeti mara baada ya kuhitimisha mafunzo hayo yaliyofanyika katika hoteli ya Edema Jijini Dodoma.